JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SEKRETARIETI YA MKOA WA MOROGORO

MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA

2020/21 – 2024/25

Imetayarishwa:-
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Boma Road
S.L.P. 650
67117 MOROGORO
Fax: 0232604988
Simu: 023 **2934305/2934306**
Baruapepe: ras@morogoro.go.tz
Tovuti: www.morogoro.go.tz

Novemba, 2020

YALIYOMO

VIFUPISHO (ABBREVIATIONS)..... iv

UTANGULIZI..... 1

1.0 MAELEZO YA UJUMLA..... 3

1.1 Mkuu wa Mkoa..... 3

1.2 Katibu Tawala wa Mkoa..... 6

2.0 DIRA, DHIMA MALENGO YA OFISI YA MKUU WA MKOA WA MOROGORO..... 8

2.1 Dira:..... 8

2.2 Dhima:..... 8

2.3 Malengo..... 8

3.0 MALENGO YA MKATABA..... 9

4.0 MAJUKUMU YA SEKRETARIETI YA MKOA WA MOROGORO..... 9

4.1 Muundo wa Sekretarieti ya Mkoa..... 10

4.2 Ufafanuzi wa Majukumu..... 11

5.0 MPANGO MAALUM WA MUDA MFUPI NA WA KATI 2020 – 2025..... 12

6.0 WATEJA WETU NA MATARAJIO..... 14

7.0 MAADILI YA WATUMISHI WA SEKRETARIETI YA MKOA..... 19

8.0 VIWANGO VYA UTOAJI HUDUMA KATIKA SEKRETARIETI..... 19

YA MKOA WA MOROGORO..... 19

9.0 MUDA WA KUSHUGHULIKIA MAJUKUMU MUHIMU:..... 21

9.1 Sehemu ya Utawala na Rasilimali watu..... 21

9.2 Sehemu ya Mipango na Uratibu..... 23

9.3 Sehemu ya Miundombinu..... 24

9.4 Sehemu ya Elimu:..... 26

9.5 Sehemu ya Huduma za Kiuchumi na Uzalishaji:..... 27

9.6 Sehemu ya Menejimenti ya Serikali za Mitaa..... 30

9.7 Sehemu ya Afya. 33
9.8 VITENGO 35
9.8.1 Kitengo cha Uhasibu na Fedha. 35
9.8.2 Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. 36
9.8.3 Kitengo cha Sheria. 37
9.8.4 Kitengo cha Ugavi. 38
9.8.5 Kitengo cha TEHAMA. 40
10.0 AHADI ZETU NA HAKI ZA MTEJA. 42
10.1 Ahadi Zetu 42
10.2 Haki za Wateja. 42
10.3 Wajibu wa wateja kwa Sekretarieti ya Mkoa 43
11.0 MAONI, MALALAMIKO NA MREJESHO WA MTEJA 43
12.0 MAPITIO YA MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA 45
13.0 MAWASILIANO: 46
14.0 KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO 47
Kitengo cha malalamiko 48
15.0 TAARIFA YA MREJESHO WA MKATABA 48
16.0 MAPITIO YA MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA 49

VIFUPISHO (ABBREVIATIONS)

1	**ASDP**	Agricultural Sector Development Programme.
2	**NGO's**	Non Government Organizations.
3	**OR – TAMISEMI.**	Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.
4	**OC**	Other Charges.
5	**OPRAS**	Open Performance Review Appraisal System.
6	**PSSSF**	Public Service Social Security Fund.
7	**RCC**	Regional Consultative Committee.
8	**TEHAMA**	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.
9	**UKIMWI**	Upungufu wa Kinga Mwilini.
10	**MSM**	Mamlaka za Serikali za Mitaa
11	**CHMT**	Council Health Management Team

UTANGULIZI

Eneo la Mkoa

Mkoa wa Morogoro una eneo la Kilometa za mraba 73,039. Eneo hili ni sawa na asilimia 7.7 ya eneo lote la Tanzania Bara ambalo ni kilomita za mraba 947,300. Kati ya eneo hili Km^2 2,240 ni maji. Mkoa umepakana na Mikoa ya Manyara na Tanga upande wa Kaskazini, kwa upande wa Mashariki unapakana na mikoa ya Pwani na Lindi, na kwa upande wa Magharibi umepakana na Mikoa ya Dodoma na Iringa. Upande wa Kusini unapakana na Mkoa wa Ruvuma.

Utawala

Mkoa wa Morogoro kiutawala umegawanyika katika Wilaya saba ambazo ni Morogoro, Mvomero, Kilosa, Kilombero, Ulanga , Gairo na Malinyi. Kufuatana na Muundo wa Serikali za Mitaa Mkoa una Halmashauri za wilaya saba (7) ambazo ni Kilosa, Mlimba, Malinyi , Morogoro, Ulanga, Mvomero, Gairo, Halmashauri ya Mji moja ya Ifakara na Halmashauri ya Manispaa moja ya Morogoro. Aidha, Mkoa unayo majimbo ya Uchaguzi 11, Tarafa 32, Kata 214, Vijiji 659, Mitaa 328, vitongoji 3,213 .



Idadi ya watu.

Kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 idadi ya watu katika Mkoa wa Morogoro ilikuwa Watu 2,218,492 kati yao Wanaume 1,093,302 na Wanawake 1,125,190. Idadi ya Kaya ilikuwa 506,275 kwa wastani wa Watu 4 katika kaya, Aidha, makisio ya idadi ya watu kwa mwaka 2020 ni watu 2,581,391 ambapo wanaume ni 1,272,143 na wanawake ni 1,309,248. kwa kiwango cha ongezeko la Watu kwa mwaka la asilimia 2.4. Hadi mwaka 2020/2025 mkoa unakisiwa kuwa na watu 2,906,388, kati yao Wanaume ni 1,432,306 na Wanawake ni 1,474,082 sawa na asilimia 51 ya watu wote.

1.0 MAELEZO YA UJUMLA

1.1 Mkuu wa Mkoa

Sekretarieti ya Mkoa ni sehemu ya Serikali Kuu kiutawala kwa mujibu wa Sheria ya Tawala za Mikoa No. 19 ya Mwaka 1997 ambayo inaelekeza majukumu na wajibu wa msingi wa shughuli za Sekretarieti ya Mkoa, Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho kwa sharia Na. 13 ya mwaka 2006

Majukumu ya Msingi ya Sekretarieti ya Mkoa ni pamoja na kuzijengea uwezo na mazingira mazuri Halmashauri zote zilizopo mkoani kwa nia ya kuziwezesha kutoa huduma nzuri kwa wananchi. Jukumu lingine ni kuwezesha kupanga mipango itakayoleta maendeleo ya haraka ya wananchi katika maeneo husika na suala la kukuza uchumi, kupiga vita umaskini na ufukara uliokithiri miongoni mwa jamii ya watanzania likiwa linapewa kipaumbele.

Sekretarieti ya Mkoa pia ni kiungo muhimu kati ya Wizara kama vile Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Taasisi, Mashirika na Asasi mbalimbali katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Msingi Mkuu wa utekelezaji wa majukumu ya Sekretarieti ya Mkoa umejengwa kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora ambapo haki za mwananchi zinazingatiwa na azma ya kutokomeza maovu yote katika jamii inaendelezwa na kudumishwa.

Sekretarieti ya Mkoa inaona umuhimu wa kuwepo na Mkataba wa Huduma kwa Mteja (Customer Service Charter) ambao ni mwongozo wa kiutendaji unaoelezea na kufafanua dira, shughuli, majukumu na malengo muhimu kwa wadau na wateja wetu. Huu ni mkataba kati ya Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro na wananchi wote wa Tanzania kwa ujumla wao.

Mkataba wetu kwa Mteja ni njia mojawapo ya kujenga uhusiano mwema na jamii ikiwa ni pamoja na kupata taarifa za mrejesho wa utendaji kazi zetu hasa zile zinazoainisha upungufu wetu kiutendaji. Mkataba huu unaashiria kuwepo na mkakati maalumu wa kuinua na kuwa na viwango vya kiutendaji katika suala zima la kutoa huduma zilizo bora kwa wateja. Mkataba huu ni makubaliano rasmi kati ya Sekretarieti ya Mkoa na wadau ama wateja wetu ambao wanapata huduma kutoka Sekretarieti ya Mkoa. Jambo la muhimu zaidi ni kujenga mazingira na uelewa hasa katika suala zima la uwajibikaji. Aidha, Mkataba huu utawawezesha wateja wa Sekretarieti ya Mkoa kuwa na matarajio ya kupata huduma nzuri.

Viwango tulivyojiwekea kwenye Mkataba huu wa Huduma kwa Mteja ni kipimo tosha cha utoaji wa huduma bora kwa kuzingatia ukweli na uwazi na uwajibikaji wa hali ya juu wa watumishi.

Ni matarajio ya Sekretarieti ya Mkoa kuwa Mkataba wa Huduma kwa Mteja utajenga hali ya kuaminiana kati ya Mteja na mtoa huduma na kufuata Sheria za nchi, Taratibu na Kanuni.

Suala la ufanisi na uwajibikaji unaozingatia maadili ni lengo kuu la Mkataba kwa Mteja, malengo yanayotekelezwa sharti yaonekane

kuwa yana dhamira ya kutoa na kutimiza wajibu kwa kutumia muda mfupi na kwa ufanisi. Haitoshi kwa Sekretarieti ya Mkoa kuwa na Mkataba kwa Mteja bila kutekeleza yale inayoahidi kufanya kwa wakati na kwa ubora na tukiwa tumeazimia kumkomboa mtanzania kutokana na maadui wakubwa wa maendeleo ambao ni Ujinga, Umaskini na Maradhi. Kazi kubwa iliyo mbele yetu ni kuunganisha nguvu za wananchi na kuelekeza nguvu hiyo kupitia Mipango ya Maendeleo ya Taifa inayoongozwa na Dira ya Taifa 2025, kwa kutumia rasilimali na fursa zilizopo ndani na nje ya Mkoa. Ni imani yangu kuwa kila mhusika katika Mkataba huu atatimiza wajibu wake ipasavyo.

Loata Erasto Ole Sanare
Mkuu wa Mkoa
MOROGORO

1.2 Katibu Tawala wa Mkoa

Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro imezindua Mkataba wa Huduma kwa Mteja kwa lengo kuu la kuweka bayana huduma zinazotolewa na viwango vya utoaji huduma hizo kwa wateja wake.

Aidha, mkataba unaonesha aina za wateja wetu, huduma wanazotarajia kupata kutoka kwetu, maadili ya watumishi wetu katika utoaji wa huduma, viwango na muda wa utoaji huduma, haki za wateja na wajibu wao katika kupata huduma. Mkataba umeweka utaratibu wa kutoa mwitikio utakaotuwezesha kutambua namna wateja wetu wanavyotuona katika utoaji wa huduma zetu, ufuatiliaji katika kuhakikisha mipango inatekelezwa kikamilifu na utaratibu wa kupokea na kushughulikia malalamiko iwapo yatajitokeza.

Katika Mkataba huu tumeonesha majukumu yetu na jinsi tulivyojipanga kuhakikisha kuwa kunakuwa na urahisi wa kupata huduma sambamba na upokeaji wa malalamiko kwa utaratibu wa haraka kwa Sehemu na vitengo vyote vya Sekretarieti ya Mkoa. Aidha, mkataba huu utaendelea kuboreshwa kadri muda unavyokwenda kwani tunatambua kukua kwa kasi kwa teknolojia nchini na duniani kote kunakochochea mabadiliko katika sekta mbalimbali za utoaji huduma na hivyo tutahakikisha kuwa mikakati ya utoaji wa huduma zetu inaendana na wakati. Lengo la Mkataba huu ni kuweka kwa uwazi huduma zetu na viwango vyetu vya utoaji huduma ambavyo wateja wetu wanaweza kuvitarajia.

Mkataba huu tunatarajia uwe kiungo rahisishi cha uhusiano wetu na wale tunaowahudumia.

Natarajia kwa kuwa na Mkataba huu wateja wetu watafurahia viwango vya huduma tutakazokuwa tunatoa kwao na wataendelea kuutumia na kutupatia mwitikio kwa lengo kuu la kuboresha ufanisi katika kazi zetu na utoaji wa huduma kwa wateja na wananchi kwa ujumla na pia kuwa kichocheo cha kuongeza ari na kasi katika utendaji wetu wa shughuli za kila siku.

Eng. Emmanuel M. Kalobelo

Katibu Tawala Mkoa

MOROGORO

2.0 DIRA, DHIMA MALENGO YA OFISI YA MKUU WA MKOA WA MOROGORO.

2.1 Dira:

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ina majukumu ya kuweka mazingira mazuri na kusimamia maendeleo katika Mkoa. Usimamizi huu unaongozwa na Dira ya Sekretarieti ya Mkoa ambayo ni kuwa ***"Taasisi ya mfano wa Kuigwa inayotoa huduma za kiuchumi na kijamii kwa kiwango cha juu".***

2.2 Dhima:

Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa kiwango cha juu kwa umma na mamlaka ya serikali za mitaa katika kutoa huduma za kiuchumi na kijamii kwa uhakika na ufanisi.

2.3 Malengo

Malengo ya utekelezaji yaliyowekwa ni:

i. Kuboresha huduma za kupunguza maambukizi ya VVU/UKIMWI,
ii. Kuendeleza, Kudumisha na kutekeleza kikamilifu Mkakati wa Taifa wa kupambana na Rushwa,
iii. Kuijengea uwezo Sekretarieti ya Mkoa ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.
iv. Kuzijengea uwezo Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kumiliki kikamilifu raslimali zilizopo kwenye maeneo yao.
v. Kuimarisha Mfumo wa usimamizi na Uratibu wa kazi za Maendeleo,

vi. Kuyashughulikia kikamilifu masuala mtambuko kuwa maendeleo endelevu ya jamii
vii. Kuyashughulikia masuala ya utawala bora,
viii. Kuimarisha huduma za Uchumi, Jamii na Miundombinu.

3.0 MALENGO YA MKATABA

Malengo Makuu ya Mkataba huu wa Huduma kwa Mteja ni:

i. Kuufahamisha umma juu ya upatikanaji, aina na viwango vya ubora wa huduma zinazotolewa na taasisi,
ii. Kubadilisha utamaduni katika utumishi wa umma kwa kuwafanya watumishi kuwa na mtazamo wa kuwajali wateja,
iii. Kuboresha utoaji huduma kwa wateja wa taasisi na wananchi kwa ujumla,
iv. Kuongeza uwajibikaji na uitikio wa watumishi katika kuwahudumia wateja kwa kuweka viwango vya huduma ambavyo tutawajibika kuvitekeleza.

4.0 MAJUKUMU YA SEKRETARIETI YA MKOA WA MOROGORO

Sekretarieti ya Mkoa inajumuisha Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Ofisi za Maafisa Tarafa. Azma ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuhakikisha kwamba inakidhi matarajio ya wananchi na hasa katika kuwawezesha na kuwajengea mazingira ya kuwaletea maendeleo ya Kisiasa, Kijamii na kiuchumi. Majukumu ya Sekretarieti za Mikoa yanatamkwa bayana katika Sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19 ya mwaka 1997 na Sheria Na. 13 ya mwaka 2006, hata hivyo bado ipo haja ya kuijengea uwezo Sekretarieti ya Mkoa ili iweze kutekeleza

majukumu yake ya msingi kwa ufanisi. Suala la kujenga uwezo kwa wataalam wake ni la lazima.

Viashiria vya maendeleo ndani ya Mkoa vitadhihirisha namna tulivyodhamiria kufanikisha malengo tuliyojiwekea, kutokana na mkakati mzima wa maendeleo ya Mkoa. Mpango wa muda mfupi na wa kati wa 2020 – 2025 unalenga kuinua huduma muhimu za kijamii, kuongeza uzalishaji mali kiuchumi, kuwa na mtandao wa maji vijijini na mijini unaowezesha wananchi wetu kupata maji kwa asilimia 85 na 95 sawia, kuwa na mtandao wa Barabara unaowezesha wananchi wetu kusafirisha mazao yao hadi kwenye masoko.

4.1 Muundo wa Sekretarieti ya Mkoa

Sekretariati ya Mkoa inaongozwa na:

i. Mkuu wa Mkoa;
ii. Katibu Tawala wa Mkoa;
iii. Makatibu Tawala Wasaidizi.

Aidha, Sekretariati ya Mkoa ina sehemu na vitengo vifuatavyo

i. Sehemu ya Mipango na Uratibu
ii. Sehemu ya Utawala na Rasilimali Watu
iii. Sehemu ya Uongozi na Usimamizi wa Serikali za Mitaa.
iv. Sehemu ya Huduma za Uchumi na Uzalishaji
v. Sehemu ya Miundo mbinu
vi. Sehemu ya Elimu

vii. Sehemu ya Afya

viii. Sehemu ya Maji

ix. Kitengo cha fedha na Uhasibu

x. Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

xi. Kitengo cha Ugavi

xii. Kitengo cha TEHAMA

xiii. Kitengo cha Sheria

xiv. Ofisi za Wakuu wa Wilaya

xv. Ofisi za Maafisa Tarafa

4.2 Ufafanuzi wa Majukumu.

4.1.1 Kuelekeza na kuratibu shughuli za maendeleo katika Mkoa.

4.1.2 Kuzijengea uwezo Serikali za Mitaa katika maeneo yafuatayo.

i. Sehemu ya Mipango na Uratibu.

ii. Sehemu ya Uchumi na Uzalishaji.

iii. Sehemu ya Miundombinu.

iv. Sehemu ya Elimu.

v. Sehemu ya Rasilimali watu.

vi. Sehemu ya Serikali za Mitaa.

vii. Sehemu ya Afya

4.1.3 Kuwezesha kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo ya Serikali za Mitaa, Fedha, Mafunzo, Mipango, Uchambuzi wa shughuli za Kiuchumi, Masuala ya Sheria, Masuala ya Rasilimali watu, Ukaguzi na Uchambuzi wa miradi.

4.1.4 Kuwezesha shughuli za uzalishaji kiuchumi ndani ya Mkoa kupitia kwa wataalam wa Kilimo, Mifugo, Ushirika, Biashara, Uvuvi na Nyuki.

4.1.5 Kuwezesha Utaalam wa kimfumo, Upimaji, Zabuni na Ukandarasi katika Sekta ya Barabara, Maji na Maendeleo ya Jamii.

4.1.6 Kuwezesha huduma za kijamii na shughuli zote za maendeleo ya Jamii zinazohusu Elimu, Afya, Maji na Ustawi wa jamii.

4.1.7 Kuhakikisha Ulinzi na Usalama ndani ya Mkoa unadumishwa.

4.1.8 Kushughulikia migogoro yote itakayowasilishwa na Serikali za Mitaa ama Umma.

4.1.9 Kuongoza vikao muhimu vya Kisheria ndani ya Mkoa.

4.1.10 Kutekeleza majukumu yote ya kikatiba yaliyokasimiwa na Wizara ama idara za Serikali.

4.1.11 Kuweka mazingira mazuri ambayo yatazihakikishia Serikali za Mitaa kutekeleza Sera za Serikali.

4.1.12 Kuelekeza na kuratibu shughuli za maafa na operesheni za msaada mkoani.

4.1.13 Kiungo kati ya Wizara, Taasisi na Asasi mbalimbali nchini.

5.0 MPANGO MAALUM WA MUDA MFUPI NA WA KATI 2020 – 2025

Mpango wa muda mfupi na wa kati umebainisha mambo muhimu ambayo yanatoa mwelekeo wa utendaji wa Sekretarieti ya Mkoa kama ifuatavyo:

5.1 Kuendelea kuijengea uwezo Sekretarieti ya Mkoa, hasa kuinua kiwango cha taaluma na ujuzi wa rasilimali watu, mfano kujaza nafasi wazi, kuongeza elimu na ujuzi.

5.2 Kujenga mazingira mazuri ya kufanyia kazi.

5.3 Kutumia rasilimali zilizopo kukidhi mahitaji yaliyokusudiwa, mfano fedha itumike kwa kuzingatia kanuni, taratibu na kwa mipango iliyokusudiwa.

5.4 Kuinua ari ya utendaji kwa wataalam.

5.5 Masuala mtambuka kujumuishwa katika mipango ya maendeleo ya Sekretarieti ya Mkoa na Serikali za Mitaa.

5.6 Kuimarisha mustakabali wa Mawasiliano (Interface) kati ya Serikali za Mitaa Mkoani, Serikali Kuu na Washirika wetu wa Maendeleo.

5.7 Kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji Mkoani.

5.8 Kuzijengea uwezo Serikali za Mitaa kukusanya mapato, kusimamia mapato na matumizi.

5.9 Kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo.

5.10 Kuratibu mapambano dhidi ya UKIMWI.

5.11 Kuimarisha vita dhidi ya Rushwa katika maeneo yote ya Mkoa wa Morogoro.

5.12 Kushirikisha Sekta binafsi na wadau mbalimbali katika kupambana na umaskini.

5.13 Kuhakikisha kwamba Mkoa unahimiza na kuelekeza suala zima la utekelezaji malengo ya maendeleo ya millennia.

5.14 Kuimarisha hali ya utulivu, amani na utengamano Mkoani.

5.15 Kuinua na kuboresha kiwango cha Elimu katika Mkoa wa Morogoro.

5.16 Kuhakikisha kwamba programu maalum ya kuendeleza kilimo zinapewa umuhimu wa pekee katika Mipango ya Mkoa.

5.17 Kuinua huduma za kijamii kama Afya, Maji Safi na Salama na Makazi bora kwa wananchi.

5.18 Kuhakikisha azma ya Serikali kufikia uchumi wa kati chini ya kauli mbiu ya **"Hapa kazi tu"** inafikiwa Mkoani Morogoro.

6.0 WATEJA WETU NA MATARAJIO

Katika Mpango Mkakati wa muda mfupi na wa kati wa Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro, tumeweza kuchambua na kuainisha wateja wetu pamoja na matarajio yao. Wateja na matarajio yao toka kwetu ni:-

WATEJA	MATARAJIO
Watumishi wa Sekretarieti ya Mkoa.	(i) Mazingira mazuri mahali pa kazi. (ii) Usalama kazini. (iii) Fursa ya kujiendeleza. (iv) Utawala bora. (v) Kupata mshahara kwa wakati. (vi) Amani, Usalama na Utulivu. (vii) Kupandishwa Vyeo. viii) Kupata mafao stahili baada ya kustaafu
Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali.	(i) Mawasiliano mazuri. (ii) Utekelezaji mzuri wa Sera Miongozo na Maelekezo. (iii) Upatikanaji wa taarifa. (iv) Upatikanaji wa mrejesho. (v) Ushauri mzuri. (vi) Amani, Usalama na Utulivu. (vii)

WATEJA	MATARAJIO
Serikali za Mitaa.	(i) Kujenga mazingira mazuri kiutendaji. (ii) Kutoa huduma nzuri kwa jamii. (iii) Kiungo kati ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu. (iv) Kupata ushauri wa kitaalam ili kutekeleza majukumu ya msingi. (v) Kuboresha mifumo ya Serikali za Mitaa. (vi) Kutafsiri na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, miongozo na maelekezo ya Serikali Kuu. (vii) Kujenga uwezo wa Serikali za Mitaa katika matumizi ya rasilimali watu, vifaa na fedha, Ushauri wa kisekta katika huduma za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Ufugaji Nyuki, Miundombinu, Sheria, Afya Elimu, Fedha, Maji, Madini na Nishati, Ardhi na Mipango Miji, Maendeleo ya Jamii, Mtandao wa Barabara Mjini na Vijijini, Uwezeshaji wananchi kiuchumi, Mawasiliano, Utawala na Utumishi, Ukaguzi, Miradi ya Maendelo, Hesabu za Halmashauri, Ushirika, Biashara na Viwanda, Rufaa kwa Maamuzi yasiyozingatia haki, Maliasili na Mazingira na Mrejesho kwa wakati. viii) Ushauri katika hesabu za fedha za Halmashauri. (ix) Ushauri katika kuandaa Bajeti za Halmashauri. (x) Ushauri kwa ajili ya kutekeleza vigezo vya kupata Ruzuku na miradi ya maendeleo. (xi) Kulinda Amani, Usalama na Utulivu.

WATEJA	MATARAJIO
Asasi zisizo za Kiserikali.	i. Kupata ushauri wa Kitaalam. ii. Kusajiliwa kwa wakati. iii. Kupata mrejesho wa taarifa. iv. Kujenga mazingira mazuri ya kufanya kazi. v. Kutambuliwa. vi. Ushirikiano na ushirikishwaji. vii. Utawala bora. viii. Sera na miongozo. ix. Amani, Usalama na Utulivu.
Jumuiya ya wafanyabiashara, Viwanda na Masoko.	i. Kuwepo na mazingira mazuri ya kufanya biashara. ii. Kushirikishwa kwenye mambo muhimu ya kimkoa au kitaifa. iii. Kuwepo kwa amani na utulivu. iv. Ushauri wa mambo ya biashara. v. Utawala bora katika uwekezaji.
Sekta Binafsi.	vi. Kupata haki ya malipo baada ya kutoa huduma. vii. Kupata haki sawa na kutoa huduma. viii. Ushirikishwaji kati ya sekta binafsi na sekta ya umma katika kutekeleza baadhi ya majukumu. ix. Kutambuliwa. x. Amani, Usalama na Utulivu.
Vyama vya Siasa.	i. Kutambua uhalali wa kuwepo Vyama vya Siasa. ii. Kushirikishwa katika mambo muhimu (Maamuzi ya kimkoa, kitaifa). iii. Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. iv. Utawala Bora.

WATEJA	MATARAJIO
	v. Kupewa haki sawa kwenye chaguzi (Demokrasia). vi. Kujenga mahusiano mazuri. vii. Amani, Usalama na Utulivu.
Vikundi vya Dini na Madhehebu.	i. Mazingira mazuri ya kuendesha shughuli zao kwa uhuru. ii. Kuheshimu uhuru wao wa kuabudu. iii. Kushirikisha dini/madhehebu katika shughuli za kiuchumi na kijamii. iv. Kutoa ushauri. v. Taratibu nzuri za kusajiliwa. vi. Kutoa haki sawa kwa madhehebu. vii. Kuidhinisha vibali vya kufanya Mikutano/mihadhara. viii. Kupata maelezo kwa hatua zilizochukuliwa kuhusu matatizo/mahitaji. ix. Amani, Usalama na Utulivu.
Vyombo vya Habari.	i. Kupata habari zilizokamilika kwa wakati Muafaka. ii. Kupata habari na matukio yote kwa uwazi na ukweli. iii. Kushirikishwa katika shughuli za maendeleo, uchumi na kijamii. iv. Kutambulika kama washirika muhimu katika maendeleo ya Mkoa. v. Amani, Usalama na Utulivu.

WATEJA	MATARAJIO
OR– TAMISEMI.	i. Kuwasilisha taarifa zilizochambuliwa kwa wakati. ii. Kutekeleza sera na maelekezo yote kwa muda Uliopangwa. iii. Utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi wa hali ya juu. iv. Kuwa na wataalamu wenye sifa na uwezo kukabili majukumu makubwa. v. Mipango mizuri ya maendeleo. vi. Kufuatilia na kuratibu utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.
Washirika wa Maendeleo.	i. Kutumia misaada yao kwa kazi zilizopangwa. ii. Kuheshimu mikataba/makubaliano. iii. Kupata taarifa inayohusu maendeleo ya Mkoa kwa wakati. iv. Kuwepo na Utawala bora. v. Kuwa na mipango mizuri ya maendeleo. vi. Kuwepo matumizi mazuri ya fedha za miradi. vii. Kuwaunganisha na Serikali za Mitaa. viii. Kuwajengea mazingira mazuri ya kufanya kazi zao. ix. Kushirikishwa na utawala bora. x. Ushauri ili kukidhi ufanisi. xi. Amani, Usalama na Utulivu.

7.0 MAADILI YA WATUMISHI WA SEKRETARIETI YA MKOA

Watumishi wa Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro wanao wajibu wa kuzingatia maadili yanayoonesha tabia njema. Maadili ya watumishi yameelekezwa katika Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 pia katika Miiko na Maadili ya Utumishi wa Umma (Ethics and Code of Conduct) na katika Sheria Na. 13 ya mwaka 1995 inayohusu Maadili ya Viongozi wa Umma ambayo inazingatia mambo yafuatayo: -

(i) Kuwa mtiifu kwa Serikali.

(ii) Kufanya kazi kwa juhudi na maarifa.

(iii) Kufanya kazi kwa umakini na ufanisi wa hali ya juu.

(iv) Ukweli na uwazi.

(v) Uadilifu.

(vi) Kuheshimu Sheria, Kanuni na Taratibu.

(vii) Kutoa taarifa sahihi.

(viii) Kutunza siri.

(ix) Kufanya kazi kama timu moja (Teamwork).

(x) Uwajibikaji.

8.0 VIWANGO VYA UTOAJI HUDUMA KATIKA SEKRETARIETI

YA MKOA WA MOROGORO

Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro inalenga kuboresha na kutoa huduma bora kwa viwango vifuatavyo:

KIWANGO	MATARAJIO
Uhusiano na wajibu kwa wateja.	Sekretarieti ya Mkoa inao wajibu wa kuendeleza na kudumisha mahusiano mema kati yake na wateja ama washirika kwa kuzingatia maslahi ya Mkoa na Taifa.
Utoaji Ushauri.	Sekretarieti ya Mkoa itaendelea kutoa ushauri makini na sahihi kwa haki sawa.
Maadili ya Watumishi.	Wakati wote Sekretarieti ya Mkoa itahakikisha kuwa watumishi wake wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia tabia njema, kujali utu, heshima na busara wakitilia maanani kwamba wao ni watumishi wa wananchi.
Muda wa kujibu hoja na mawasiliano.	Sekretarieti ya Mkoa kila mara kwa wakati wote itashughulikia masuala yote pamoja na dharura, malalamiko yote, hoja zote kwa haraka.
Ubora.	Sekretarieti ya Mkoa itahakikisha kwamba barua zote na mawasiliano yanafanywa kwa usahihi na lugha nyepesi inayoeleweka.
Umakini/ufasaha na usahihi.	Sekretarieti ya Mkoa itahakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakidhi mahitaji na matarajio ya wateja/washirika kwa usawa na kuzingatia makundi maalumu hasa watoto, wanawake na walemavu.

9.0 MUDA WA KUSHUGHULIKIA MAJUKUMU MUHIMU:

9.1 Sehemu ya Utawala na Rasilimali watu.

Na	Huduma	Muda
9.1.1	Kufikisha majalada kwa Maafisa wanaohusika.	Dakika 30
9.1.2	Kushughulikia barua zinazowasili na kutoka.	Siku 3
9.1.3	Kukamilisha taratibu za ajira kwa watumishi wapya walioripoti baada ya kupangiwa vituo vya kazi na Sekretarieti ya Ajira pamoja na kushughulikia ujazaji wa nafasi wazi.	Siku 10
9.1.4	Kusikiliza na kushughulikia malalamiko.	Siku 14
9.1.5	Kutoa vibali mbalimbali kwa wateja mfano utafiti, likizo, ruhusa, vibali vya kustaafu, kuacha kazi n.k.	Siku 3
9.1.6	Kuandaa Stahili za Waatumishi na kuwasilisha kwenye mamlaka husika mafano mirathi, pensheni, kiinua mgongo, Mishahara ya Watumishi, Malimbikizo ya mishahara.	Siku 7
9.1.7	Kukamilisha maandalizi ya Bajeti ya Mishahara na kuiwasilisha Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Hazina.	Siku 14
9.1.8	Kutayarisha taarifa za utekelezaji wa taarifa mbalimbali kama vile taarifa za matukio, taarifa za Kiutumishi na kuwasilisha kwenye Mamlaka husika kulingana na mahitaji yake.	Kila robo mwaka
9.1.9	Kujibu hoja za Kaguzi mbalimbali zinazofanyika katika Sekretarieti ya Mkoa.	Siku 14

Na	Huduma	Muda
9.1.10	Kusimamia ujazaji wa fomu za OPRAS na kukamilisha upimaji wake.	Siku 7
9.1.11	Kushughulikia maombi ya vibali vya ajira ya Wataalam wa Kigeni baada ya kupata maombi kutoka kwenye taasisi mbalimbali na kuwasilisha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora	Siku 14
9.1.12	Kuandaa mpango kazi wa Sehemu.	Siku 2
9.1.13	Kuandaa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida (OC)	Siku 2
9.1.14	Kufanya uchunguzi wa mambo mbalimbali na kutoa taarifa/matokeo ya uchunguzi.	Siku 14
9.1.15	Kuandaa vikao mbalimbali vya Kisheria.	Siku 2
9.1.16	Kutoa taarifa za Maafa/Majanga.	Siku 1
9.1.17	Kuhudumia Wateja.	Siku 1
9.1.18	Kuandaa muhtasari wa vikao vya kisheria.	Siku 3
9.1.19	Usimamizi na ufuatiliaji.	Kila siku
9.1.20	Kusimamia na kuratibu Shughuli za Maandalizi ya Mwenge wa Uhuru	Siku 90
9.1.21	Kusimamia masuala ya usafiri na kutoa vibali vya safari za ndani na nje	Kila siku
9.1.22	Kusimamia Usafi wa Mazingira	Kila siku
9.1.23	Kusimamia Mpango wa Mafunzo kwa Watumishi	Kila siku
9.1.24	Kusimamia maandalizi ya ugeni wa Kitaifa, Itifaki n.k	Siku 7
9.1.25	Kujibu barua.	Siku 3

Na	Huduma	Muda
9.1.26	Makatibu Tawala Wilaya kusajili ndoa	Siku 24
9.1.27	Makatibu Tawala Wilaya kusajili Vizazi	Siku 7
9.1.28	Makatibu Tawala Wilaya kusajili Vifo	Siku 3

9.2 Sehemu ya Mipango na Uratibu

Na	Huduma	Muda
9.2.1	Kuandaa majibu ya maswali ya Bunge.	Siku 7 baada ya kupokelewa
9.2.2	Usambazaji wa Miongozo ya Bajeti kwa Halmashauri za Wilaya.	Siku 2 baada ya kuwasili
9.2.3	Kujibu hoja za ukaguzi.	Siku 3
9.2.4	Ukaguzi na tathmini ya Miradi katika Serikali za Mitaa na Sekretarieti ya Mkoa, kila robo mwaka.	Siku 14
9.2.5	Kuandaa muhtasari wa kikao cha RCC.	Siku 3
9.2.6	Kushughulikia usajili wa Asasi zisizo za Kiserikali (NGOs).	Siku 3
9.2.7	Kuandaa Bajeti ya matumizi ya kawaida (OC).	siku 14
9.2.8	Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati (Strategic Plan).	Siku 21
9.2.9	Kuwasilisha utekelezaji wa Bajeti ya Mkoa.	Siku 14
9.2.10	Kuandaa na kuwasilisha Hazina Mpango wa muda mfupi na wakati wa Bajeti ya Mkoa.	Machi - Aprili kila mwaka
9.2.12	Kupitia Bajeti za Halmashauri.	Siku 4

Na	Huduma	Muda
9.2.13	Kuandaa na kuratibu vikao vya RCC.	Siku 14
9.2.14	Kumhudumia mteja.	Siku 1
9.2.15	Kuandaa na kuwasilisha taarifa za robo mwaka na mwaka.	Siku 14
9.2.16	Kuandaa muhtasari wa vikao vya kisheria.	Siku 3
9.2.17	Kukiri mapokezi ya barua	Siku 1
9.2.18	Kujibu barua tangu kupokelewa	Siku 2
9.2.19	Kuandaa taarifa za kikao.	Siku 7
9.2.20	Usimamizi na ufuatiliaji wa miradi.	Siku 14
9.2.21	Kushughulikia malalamiko ya wananchi	Siku 14

9.3 Sehemu ya Miundombinu

Na	Huduma	Muda
9.3.1	Kuandaa taarifa za robo Mwaka na vikao vya Kisheria (RCC) na Bodi ya Barabara.	Siku 7
9.3.2	Kutoa ufafanuzi wa Sheria, Kanuni, Sera na Miongozo kwa Serikali za Mitaa na wadau wengine.	Siku 7
9.3.3	Kufanya Ukaguzi wa Miradi katika Halmashauri.	Siku 14
9.3.4	Kufanya mapitio ya Usanifu wa miradi.	Siku 7
9.3.5	Kufanya ukaguzi wa kazi za upimaji na michoro ya Mipango Miji kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa.	Siku 7
9.3.6	Kujibu barua na hoja za sekta ya Miundombinu	Siku 5
9.3.7	Kuandaa Bajeti ya kawaida (OC) na Bajeti ya	Siku 3

Na	Huduma	Muda
	miradi ya maendeleo ya sekta ya Miundombinu.	
9.3.8	Kufuatilia taarifa za utekelezaji wa shughuli za Sekta za Miundombinu katika Mamlaka za Serikali za mitaa na Taasisi za Serikali zinazojitegemea.	Siku 7
9.3.9	Kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Sekta za Miundombinu.	Siku 14
9.3.10	Kuandaa nyaraka (Makisio) kwa ajili ya kutafuta Wakandarasi wa shughuli za ujenzi.	Siku 14
9.3.11	Kukagua na kuandaa taarifa za tathmini ya mazingira "Environmental Impact Assessment Report" **(EIA).**	Siku 7
9.3.12	Kuandaa taarifa za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwa sekta za Miundombinu.	Siku 7
9.3.13	Kukiri mapokezi ya barua tangu kupokelewa.	Siku 1
9.3.14	Kuandaa na kuwasilisha taarifa za robo mwaka na mwaka.	Siku 14
